# HALMASHAURI YA MJI WA MBULU

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA KILICHOFANYIKA TAREHE 22.10.2021 KWENYE UKUMBI WA HALMASHAURI.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| Na. | Jina | Kata/Jimbo | Wadhifa. |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Peter M. Sulle | Diwani Kata ya Sanu | Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. Yefred Myenzi | Mkurugenzi wa Mji wa Mbulu | Katibu |
| 3. | Mhe. Alex A. Tango | Diwani Kata ya Gehandu | M/Mwenyekiti |
| 4. | Mhe. Basil Boay | Diwani Kata ya Imboru | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Anthon J. Genda | Diwani Kata ya Tlawi | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Emanuel A. Burra | Diwani Kata ya Murray | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Elizabeth A. Bayyo | Diwani Vitimaalum | Mjumbe |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

| Na. | Jina | Kata/Jimbo | Wadhifa. | Sababu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Zacharia P. Isaay | Mbunge Mbulu Mjini | Mjumbe | kwa taarifa |
| 2. | Mhe. Yustina Rahhi | Mbunge Vitimaalum | Mjumbe | Kwa taarifa |

**WATENDAJI WALIOHUDHURIA**

| Na. | Jina | Cheo |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Bakarani H. Urio | Afisa Utumishi na Utawala (M) |
| 2. | Ndg. Hillary G. Makundi | Afisa Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji (M) |
| 3. | Ndg. Vicent Mugeta | Afisa Usafi na Mazingira (M) |
| 4. | Ndg. Omary Mandia | Mhasibu |
| 5. | Ndg. Batilda V. Genda | Afisa Utumishi |
| 6. | Ndg. Simon Liachema | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi |
| 7. | Ndg. Magoti Sijaki | Afisa Ushirika |
| 8. | Ndg. Philemon Maffa | Kaimu Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji (M) |
| 9. | Ndg. John Kajivo | Mkaguzi wa Ndani |
| 10. | Ndg. MacDonald Tsere | Afisa Mazingira |
| 11. | Ndg. Mary Mazengo | Afisa Dawati la Malalamiko |
| 12. | Ndg. Joseph Kimaro | Afisa Misitu na Maliasili |
| 13. | Ndg. Jovin Didace | Kaimu Afisa Sheria |
| 14. | Ndg. Elianor Nkata | Kaimu Afisa Elimu Sekondari (M) |
| 15. | Ndg. Mhumpa S. L | Afisa Manunuzi |
| 16. | Ndg. Gladness Msuya | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (M) |
| 17. | Ndg. Annamary Galibona | Afisa Maendeleo ya Jamii (M) |



CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 18. | Ndg. Joseph Geheri | Afisa Uchaguzi |
| 19. | Ndg. Sara E. Sanga | Katibu Tawala Wilaya |
| 20. | Ndg. Irene Ringo | Afisa Ustawi wa Jamii |
| 21. | Ndg. Michael Longole | Afisa Biashara |
| 22. | Ndg. Veronica Mao | A/TSC |
| 23. | Ndg. Exsupery Aloyce | Kaimu Afisa Elimu Msingi (M) |
| 24. | Ndg. Fatuma Abdalah | Mchumi |
| 25. | Ndg. Keretho Laizer | Mhasibu wa Mapato |
| 26. | Ndg. Marcely Lusinge | Katibu wa Afya |
| 27. | Ndg. Dominic Tembe | Afisa TEHAMA |
| 28. | Ndg. Christopher Nyalu | Mganga Mkuu |
| 29. | Ndg. Kingo Makumbuli | Mratibu wa TASAF |
| 30. | Ndg. Dickson Kusenha | Afisa Mipango Miji na Vijiji |

**SEKRETARIETI**

| Na. | Jina | Cheo. |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Patrick Mwinuka | Katibu wa Kamati za Halmashauri |
| 2. | Ndg. Ester Emmanuel | Katibu wa Kamati za Halmashauri |

**MUHT.Na.248/FU/10/01/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Akidi ya wajumbe ilipotimia katibu alimkaribisha Mh.Mwenyekiti ili afungue kikao. Mh.Mwenyekiti alianza kwa kuwashukuru wajumbe wote kwa mahudhurio, na kumshukuru Mungu kwa afya aliyowajalia wajumbe na kuweza kuhudhuria kikao. Pia alitoa pongezi kwa menejimenti kwa utendaji kazi mzuri unaojidhihirisha kwenye mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa mapato. Aliwashukuru pia waheshimiwa madiwani kwa kumpa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Halmashauri. Baada ya kusema hayo Mh.Mwenyekiti aliwaomba wajumbe na wataalam kutoa ushirikano katika agenda za kikao na kutamka kufungua kikao rasmi mnamo saa 4:28 za asubuhi.

**MUHT.Na.249/FU/10/02/2021: KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO**

Wajumbe waliafiki agenda zifuatazo kujadiliwa katika kikao hicho: -

1. Kufungua Kikao
2. Kuridhia dondoo za kikao tarehe 22.10.2021
3. Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala cha tarehe 21.09.2021
4. Yatokanayo na kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala cha tarehe 21.09.2021
5. Mapendekezo ya miradi ya maendeleo itakayopata fedha ya mapato ya ndani.
6. Fedha zilizotengwa kutokana na mpango wa maendeleo ya ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya uviko 19 kwenye Halmashauri ya Mji wa Mbulu Oktoba 2021



CamScanner

7. Taarifa mbalimbali za utekelezaji wa idara na vitengo mbalimbali kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba 2021/22
   - (i) Taarifa ya Mapato na Matumuzi
   - (ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo
   - (iii) Taarifa ya Manunuzi
   - (iv) Taarifa ya Ukaguzi wa Ndani
   - (v) Taarifa ya Sheria
   - (vi) Taarifa ya Utawala na Utumishi
8. Bango la Mkurugenzi
9. Mengineyo kwa idhini ya Mheshimiwa Mwenyekiti.
10. Kufunga kikao.

**MUHT.Na.250/FU/10/03/2021: KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 21.09.2021.**

**Makamu Mwenyekiti Mh. Alex Tango** aliwapitisha wajumbe kwenye muhtasari wa kikao cha tarehe 21.09.2021 ukurasa kwa ukurasa. Muhtasari haukuwa na masahihisho yoyote hivyo wajumbe walijadili na kuridhia usainiwe kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

**MUHT.Na.251/FU/10/04/2021: YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA CHA TAREHE 21.09.2021.**

Kikao kilipokea taarifa ya utekelezaji wa maazimio matano kutokana na muhtasari wa kikao kilichopita kama ifuatavyo:

**Azimio Na. 1.** Orodha ya vyanzo vyote, tozo zake, na wakusanyaji wake iandikwe na kuwasilishwa kwa kuzingatia kiasi cha fedha kinachotakiwa kukusanywa. Aidha, pawepo na wasimamizi kwa kila kata kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia utekelezaji katika ukusanyaji wa mapato. **Mweka hazina** aliwasilisha taarifa yenye orodha ya vyanzo vyote iliwasilishwa pamoja na walezi wa kila kata kama ilivyoazimiwa na kupokelewa.

**Azimio Na. 2.** Mchanganuo wa mgawanyo wa fedha za miradi ya mapato ya ndani kwa miezi yote iliyobaki uwasilishwe. **Afisa Mipango** aliwasilisha mchanganuo wa fedha za miradi kwa mwezi husika na akaeleza kuwa mchanganuo wa miezi mingine utategemea makusanyo ya mwezi husika. Taarifa hiyo ilipokelewa.

**Azimio Na. 3.** Tangazo la kuwataka wafanyabiashara na wamiliki wa magari ya mizigo kupaki katika eneo husika lirudiwe na kutangazwa kupitia Radio Habari Njema baada ya



CamScanner

kufanyiwa maboresho ili taarifa ziwafikie wananchi wengi zaidi. **Afisa Manunuzi** aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa azimio hilo na taarifa ilipokelewa.

**Azimio Na. 4.** Ufuatiliaji wa wafanyabiashara wanaozunguka eneo la stendi kuu ya mabasi ya Mbulu Mjini wanaofanya biashara pasipokuwa na mkataba na halmashauri ufanyike na kuhakikisha wote wanasaini mikataba. **Mwanasheria** aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa azimio hili ambapo wafanyabiashara 52 kati ya 65 walishasaini mikataba. **Mh. Anthon Genda** alipongeza jitihada zilizofanyika na menejimenti na kusisitiza kuwa waliobaki wafuatiliwe ili wote wasaini mikataba. **Mwenyekiti wa Halmashauri** alihitimisha hoja kwa kupongeza menejimenti na kuwataka waendelelee na jitihada kama hizo kwenye vyanzo vingine vya mapato.

**Azimio Na. 5.** Wajumbe wa kamati ya fedha na utawala wafanye ziara ya kukagua miradi iliyopendekezwa ili kuona utekelezaji. **Menejimenti** ilishauri kuwa Kamati ifanye ziara baada ya utekelezaji wa miradi kufikia hatua zinazoridhisha. **Mwenyekiti wa Halmashauri** aliunga mkono hoja na kupendekeza kuwa kamati ifanye ziara kwenye miradi iliyobakia wakati wa ziara ya kukagua miradi mwaka uliopita. Wajumbe waliunga mkono pendekezo hilo na kuazimia menejimenti ipange muda muafaka wa kutembelea miradi hiyo.

**MUHT.Na.252/FU/10/05/2021: MAPENDEKEZO YA MIRADI YA MAENDELEO YA KUPELEKEWA FEDHA ZA MAPATO YA NDANI.**

Afisa Mipango aliwasilisha orodha ya miradi ya maendeleo iliyopelekewa fedha za mapato ya ndani yenye thamani ya **Tsh. 86,600,000.** kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2021. Baada ya mawasilisho **Mh. Anthon Genda** alipongeza Menejimenti kwa kupeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo na kutaka utaratibu huo uendelee kila mwezi na kwa kuzingatia uwiano wa kata zote. Hoja hiyo iliungwa mkono na Mh. Basil Boay ambaye alitaka jitihada zaidi zielekezwe kwenye ukusanyaji wa mapato ili fedha nyingi ziende kwenye miradi. **Mh Mwenyekiti wa Halmashauri** alihitimisha hoja kwa kushauri menejimenti itoe kipaumbele kwa Kata ambazo zimepokea fedha kidogo za miradi kutoka serikali kuu badala ya kulimbikiza fedha za mapato ya ndani na za ruzuku ya serikali kuu kwenye kata moja.

**MUHT.Na.253/FU/10/06/2021: MGAO WA FEDHA KUTOKANA NA MPANGO WA MAENDELEO YA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO 19 KWENYE HALMASHAURI YA MJI WA MBULU.**



CamScanner

**Mkurugenzi wa Halmashauri** aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri ya Mji wa Mbulu imetengewa fedha kiasi cha **Tsh. 860,000,000.** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kijamii kutokana na mgao wa fedha za mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO 19. Alieleza kuwa fedha hizo zimeelekezwa kwenye sekta za Elimu na Afya. Kwa upande wa sekta ya elimu fedha hizo zimeelekezwa katika ujenzi wa madarasa ishirini ya shule za sekondari na nane kwa shule shikizi. Jumla ya fedha zilizoelekezwa kwenye ujenzi wa madarasa hayo ni **Tsh. 560,000,000.** Kwenye sekta ya afya, fedha hizo zimeelekezwa katika ujenzi wa jengo la huduma za dharura "*Emergency Medical Department*" (EMD) linalotarajiwa kugharimu **Tsh.300,000,000. Mkurugenzi wa Halmashauri** aliomba kamati ya Fedha na Utawala iridhie fedha hizo ziingizwe kwenye bajeti ya Halmashauri na kupangiwa vifungu ili ziweze kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Baada ya mawasilisho hayo wajumbe wote kwa pamoja waliipokea taarifa, wakaishukuru serikali kwa kutoa fedha hizo kwa Halmashauri kisha kuridhia fedha hizo zipangiwe vifungu kwa ajili ya matumizi. **Mh. Mwenyekiti wa Halmashauri** alihitimisha hoja hii kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyotekeleza majukumu na kuwajali wananchi wakiwemo wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Aliitaka menejimenti kusimamia fedha hizo na kutoa taarifa kwenye kila kata ambako miradi hiyo itatekelezwa ili waheshimiwa madiwani waweze kushiriki kufanya ufuatiliaji.

**MUHT.Na.254/FU/10/07/2021: TAARIFA MBALIMBALI ZA UTEKELEZAJI WA IDARA NA VITENGO KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA JULAI – SEPTEMBA 2021**

**1. IDARA YA FEDHA**

**Mweka Hazina** aliwasilisha taarifa ya mapato kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2021 ya kiasi chaTsh. 4,935,048,056.70 sawa na asilimia 22% ya lengo kwa mwaka na matumizi ya Tsh. 4,437,535,235.40 sawa na asilimia 20% ya lengo kwa mwaka. Aidha taarifa ilionesha kuwa mapato ya ndani yalikuwa Tsh. 450,705,370 sawa na asilimia 35 na matumizi ya Tsh. 412,014,529.67 sawa na asilimia 32. Wajumbe waliipokea taarifa hiyo wakajadili na kuipongeza menejimenti kwa kuongeza makusanyo ya ndani. **Mh. Alex Tango** alisisitiza kuwa jitihada hizi zinastahili pongezi lakini menejimenti ijielekeze kwenye vyanzo ambavyo asilimia ziko chini. Hoja hiyo iliungwa mkono na **Mh. Basil Boay na Mh. Anthon Genda** ambao walisisitiza mikakati ya ukusanyaji mapato kwenye vyanzo kama vile ushuru wa samaki, vibali vya kusafirisha Nguruwe, na tozo za usafi



CamScanner

iongezwe. Wajumbe hao walisisitiza kuwa mkakati maalumu uwekwe kwa ajili ya kuongeza makusanyo kwenye vyanzo vyote viliyokusanywa chini ya asilimia 10. Baada ya mjadala huo, **Mh.Mwenyekiti wa Halmashauri** alihitimisha hoja kwa kuelekeza menejimenti ije na mkakati kwenye kikao kijacho wa jinsi ya kuongeza makusanyo kwenye vyanzo hivyo.

## 2. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Afisa Mipango** aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo Halmashauri imeidhinishiwa **Tsh 3,657,698,350** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka vyanzo vitano ambavyo ni Mapato ya ndani Tsh. 266,940,000.00, Serikali Kuu Tsh.1,324,610,350 EP4R Tsh. 693,163,000 Miradi ya SEQUIP Tsh.1,328,400,000 na Mfuko wa Jimbo Tsh. 44,585,000. Baada ya mawasilisho hayo wajumbe walishauri pawepo na uwazi katika utekelezaji wa miradi. Pamoja na ushauri huo, kikao kiliagiza mchanganuo **Tsh. 500,000,000** za ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya Hospitali ya mji uwasilishwe katika kikao kijacho. Taarifa hiyo ilipokelewa na kupitishwa.

## 3. TAARIFA YA KITENGO CHA MANUNUZI

Afisa Manunuzi aliwasilisha taarifa ya Kitengo cha manunuzi na ugavi kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2021 iliyoonesha kuwa Halmashauri imefanya manunuzi yenye thamani ya Tsh. 43,045,702 kupitia idara zake mbalimbali kama ifuatavyo; idara ya utawala Tsh. 20,224,000.00, idara ya elimu msingi Tsh.13,934,962, kitengo cha ukaguzi wa ndani Tsh 242,700.00, idara ya afya Tsh 1,314,520, na idara ya maendeleo ya jamii Tsh 7,329,520. Baada ya mawasilisho hayo kikao kiliagiza menejimenti ifanye mchakato mwingine wa kutangaza tenda ya kuuza miti katika msitu wa Quru na Umi ili kufikia malengo ya Halmashauri. Pia kikao kilishauri kuwa ni vyema matengenezo ya gari la idara ya fedha na gari la kubebea taka ngumu yazingatiwe na kupewa kipaumbele.
Taarifa hiyo ilipokelewa na kupitishwa.

## 4. UKAGUZI WA NDANI

**Mkaguzi wa Ndani** aliwasilisha taarifa ya kitengo cha ukaguzi wa ndani iliyokua na hoja tatu katika kipindi cha Julai 1 – Septemba 30, 2021. Hoja hizo Malipo yasiyokuwa na viambatisho Tsh.1,725,000, Kutotumika kwa wakati chanjo za mifugo, na kukosekana kwa mikataba 12 ya vibanda vinavyozunguka stendi ya mabasi ya Mbulu mjini. Pamoja na mawasilisho hayo, ufafanuzi wa hoja hizo ulitolewa na maagizo ya kuwasilisha viambatisho, na kuwachukulia hatua za kisheria wote ambao wamekiuka masharti ya



CamScanner

upangaji yazingatiwe. Pia ushauri wa kufanya tafiti kwanza ili kujua hitaji, aina ya chanjo, na kiasi cha chanjo kinachohitajika ili kuepuka hasara zinazoweza kujitokeza ulitolewa kwa idara ya mifugo na kupokelewa. Taarifa hiyo ilipokelewa na kupitishwa.

## 5. KITENGO CHA SHERIA

**Mwanasheria** aliwasilisha taarifa ya hali ya kesi zilizopo katika mahakama mbalimbali kwa mwezi Septemba 2021, pamoja na hali halisi ya utekelezaji wa majukumu mengine ya kushughulikia uundwaji wa mabaraza ya ardhi, kuwasilisha orodha ya majina ya wazee wa mahakama za mwanzo, kufuatilia nakala za sheria ndogo, na ukusanyaji wa mapato. Baada ya mawasilisho hayo **Mhe. Anthon Genda** alishauri kuwa ni vyema menejimenti ikafanya jitihada za kupunguza wingi wa kesi zilizopo mahakamani kwa njia ya mazungumzo (ADR). **Mwenyekiti wa Halmashauri** alihitimisha hoja hiyo na taarifa ilipokelewa na kupitishwa.

## 6. IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA

**Afisa Utumishi na Utawala** aliwasilisha taarifa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya idara kwa mwezi Septemba 2021, yakiwemo usimamizi wa utekelezaji wa idara 13 na vitengo 6 vya Halmashuari, pamoja na usimamizi na utekelezaji wa majukumu na mahitaji mbalimbali ya watumishi kama likizo, mishahara, uhamisho, watumishi waliostaafu, watumishi waliobadilishiwa vituo vya kazi, watumishi waliopo masomoni, stahiki za waajiriwa wapya katika kada mbalimbali, mapambano dhidi ya rushwa, na mapendekezo na mikakati ya utatatuzi wa changamoto zinazokabili idara. Baada ya mawasilisho **Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri** alisisitiza msawazisho wa ikama uzingatie hitaji la walimu katika shule zenye upungufu. Na kuwepo na usimamizi wa ufanyikaji wa vikao vya kisheria kwenye ngazi za chini pamoja na usomaji wa taarifa za mapato na matumizi. **Mwenyekiti wa Halmashauri** alihitimisha hoja hiyo na taarifa ilipokelewa na kupitishwa.

## MUHT.Na.255/FU/10/08/2021: BANGO LA MKURUGENZI

**Mkurugenzi wa Halmashauri** aliwasilisha taarifa za kiutawala zikiwemo ufanyikaji wa vikao vya kisheria; vikao vya ALAT mkoa na Taifa, uhaba wa watumishi, ombi la halmashauri la kupewa fedha kwa ajili ya kujenga jengo la utawala, maboresho ya jengo kukidhi mahitaji muhimu, taarifa ya ufanyikaji wa semina kwa waheshimiwa madiwani, uharibifu wa mazingira, usikilizaji wa kero za wananchi, mahusiano baina ya Halmashauri na taasisi nyingine, mwenendo wa ukusanyaji wa mapato, mikakakti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na maagizo na maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na viongozi. Baada ya mawasilisho hayo wajumbe walipongeza taarifa hiyo na kuipokea.



CamScanner

**MUHT.Na.256/FU/10/09/2021: MENGINEYO**

Katika mengineyo **Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri** aliagiza ufuatiliaji katika maeneo yafuatayo: - maghala yaliyopo Laghandamur na Gehandu yafuatiliwe ili kujua kama yanafanya kazi na kama vijiji husika vinafaidika na maghala hayo. Menejimenti ilielekezwa kubainisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya malipo ya madiwani zitaelekezwa kutekeleza miradi gani baada ya malipo hayo kuwa yanafanywa na serikali kuu. Ufuatiliaji wa fedha za faini walizolipa wavuvi ufanyike ili kujiridhisha kama fedha hizo zimepelekwa benki. Na maelekezo kutoka kwenye ofisi ya Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya kusimamia miradi na kuwajulisha wananchi juu ya miradi hiyo ili kupata ushiriki wao pindi itakapohitajika yalitolewa na kupokelewa.

**MUHT.Na.257/FU/10/10/2021: KUFUNGA KIKAO.**

**Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri** alipongeza menejimenti kwa utekelezaji mzuri katika ukusanyaji wa mapato, na kuwashukuru wajumbe kwa michango yao katika agenda za zilizowasilishwa. Baada ya kusema hayo, mwenyekiti alitamka kufunga kikao rasmi saa 8:24 za mchana.

ULITHIBITISHWA NA;

JINA: YEFRED MYENZI — JINA: PETER M. GULLE

SAINI: [signature] — SAINI: [signature]

KATIBU — MWENYEKITI

TAREHE: 23/11/2021

[signature]